

Uzingativu wa Utamaduni katika Utayarishaji wa Matini Halisi za Kujifunzia Lugha ya Pili

Asia Mashaka Akaro
Taasisi ya Elimu Tanzania
asiagm2015@gmail.com

Ikisiri

Utafiti huu unachunguza umuhimu wa Matini Halisi zinazoakisi utamaduni wa lugha husika katika kujifunza Lg2. Utafiti huu ni wa kimaktaba. Mbinu ya ukusanyaji wa data iliyotumika ni uchanganuzi wa nyaraka. Data za msingi zilikusanywa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Utafiti huu umebaini kuwa Matini Halisi za kufundishia Lg2 lazima ziwe zimezingatia mazingira yanayohusika ambamo zitatumika na zichochee maingiliano na uzalifu. Pia, zizingatie maumbo na dhima ya Lg2 na shurti zifungamanishe stadi zote za lugha za kusikiliza, kuzungumza, kusoma, kuandika na utamaduni. Kwa upande wa mchango wa Matini Halisi zilizozingatia utamaduni wa lugha lengwa, mjifunzaji Lg2 anahusisha moja kwa moja matini anayoitumia na kitu anachojifunza. Mjifunzaji anapata uelewa wa kujieleza kwa urahisi na anajifunza kwa urahisi misamiati mipya kupitia maelezo au ufafanuzi uliomo katika matini hizo. Mjifunzaji wa Lg2 anapata motisha ya kujifunza kupitia mtini hizo. Mjifunzaji wa Lg2 hukuza stadi za lugha katika hali ya ung'amuzitambuzi. Makala yamehitimisha kwamba ili matini halisi ziwe na tija kwa wajifunzaji shurti ziwe nyumbufu na kwenda na wakati.

Maneno Msingi: Matini Halisi, Uhalisi wa Matini, Uhalisi wa Matini Kiuendelevu na Uhalisi wa Matini Kimatumizi.

Utangulizi

Miongoni mwa vifaa muhimu vya mwalimu wa Lg2 ni matumizi ya matini anuai darasani. Matini hizo zinaweza kuwa ni zile zilizoandaliwa rasmi kwa ajili ya kufundishia Lg2. Matini ambazo kwa asili hazikuandaliwa kwa ajili ya kutumika kufundishia wanafunzi wanaojifunza Lg2, lakini mwalimu wa lugha anapozitumia kama nyenzo mojawapo ya kuwasilishia maudhui kwa wanafunzi wa lugha. Katika taaluma ya isimutumizi ndizo hujulikana kama Matini Halisi. Matini ambazo hutayarishwa maalumu kwa ajili ya watumiaji wazawa wa lugha husika. Kwa mfano, nyimbo, magazeti au vitabu. Mjifunzaji wa Lg2 anapofundishwa kwa kutumia matini

MAKALA HALISI

HISTORIA YA MAKALA

Kupokelewa: 15 Julai 2021

Kurekebisha: 19 Sept. 2021

Kukubaliwa: 29 Oktoba 2021

Kuchapishwa: 08 Dis. 2021

ISSN: 2453 – 6016

Juzuu 7,

Toleo 2,

pp. 53 – 61.

NUKUU: Akaro, A. M. (2021). Uzingativu wa Utamaduni katika Utayarishaji wa Matini Halisi za Kujifunzia Lugha ya Pili. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences*, 7(2), 56 – 64.

hizi huipata lugha inayohusika katika uasili wake. Kazi muhimu ya kutumia vifaa darasani ni kuwezesha fursa ya ujifunzaji kutendeka. Rubin (1979) anasema ujifunzaji mzuri wa lugha unategemo mtazamo, motisha na fursa.

Kwa upande wa fursa, hujumuisha vifaa na shughuli zote ndani na nje ya darasa ambazo humchangamanisha mjifunzaji na lugha. Kujifunza lugha yoyote ni kwa ajili ya kutaka kufanya mawasiliano na wazawa wa lugha hiyo (Grellet, 1981). Dhima ya Matini Halisi katika ujifunzaji wa Lg2 zimeibua kambi mbili zinazosigani. Kambi ya kwanza ikiongozwa na Gilmore (2007) na Rilling na Dantas-Whitney (2009) wanadai kuwa Matini Halisi zinafaa kutumika katika kufundisha lugha kwa kuwa huibua ingizo la kiisimu kwa wajifunzaji. Matini Halisi huleta tajiriba nzuri ya utumiaji wa lugha kwa kuwa huwahamasisha wajifunzaji kujifunza lugha hiyo kutokana na vionjo vya kiutamaduni vilivyofumbatwa na matini hizo na kuwajengea uwezo wa kuwasiliana.

Kambi ya pili ya wanaisimu ikiongozwa na Ellis (1999) wanadai kuwa Matini Halisi hazifai kutumika kujifunzia Lg2 kwa kuwa zinaweza kuwapa ugumu wajifunzaji. Kundi hili linapinga zisizitumike katika ufundishaji lugha badala yake wanapendekeza kutumia matini za kutengenezwa mahususi kwa ajili ya kufundishia Lg2. Pamoja na msigano huo kuhusiana na Matini Halisi, dhima yake katika muktadha wa darasa la lugha hauwezi kupuuzwa. Ushuhuda uliobainishwa na Pinner (2015) ni muhimu sana kuutaja hapa. Matini Halisi zinaweza kuwa kitu chenye nguvu sana kwa kumnyanyua mjifunzaji na mwalimu kwa sababu Matini Halisi zinamuunganisha mjifunzaji binafsi na maudhui yanayotumika kujifunzia. Muunganiko huu bila shaka ni muhimu pia kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Hivyo, utafiti huu unachunguza umuhimu wa Matini Halisi zinazoakisi utamaduni wa lugha husika katika kujifunza Lg2.

Mbinu za Utafiti

Mbinu ya ukusanyaji wa data iliyotumika ni uchanganuzi wa nyaraka. Utafiti huu ni wa kimaktaba. Data za msingi zilikusanywa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina maktaba ya kisasa iliyowezesha kupatika kwa nyaraka muhimu zilizohitajika katika makala hii. Katika kuhakikisha lengo la utafiti huu linafikiwa, utafiti ulichanganua miongozo ya utayarishaji wa Matini Halisi kama ilivyopendekezwa na Jordan (2012) na Pinner (2014). Miongozi hii ilichaguliwa kwa sababu ni miongozo jumuishii na hivi karibuni. Katika maoni yao, wataalamu hawa walipendekeza sifa moja wapo ya Matini Halisi ni uwezekano wa kubadilika kimatumizi kwa kuzingatia muktadha na wajifunzaji wa Lg2. Uhalisi wa matini si tuami bali ni jongevu. Jordan kwa upande mwingine anaeleza kuwa Matini Halisi hazitarajiwi kuwa na mwanmda funyu bali ziwe za kisasa na zenye mawanda mapana. Matini Halisi zinatarajiwa kuwa za kisasa na zinazozingatia utamaduni wa lugha husika.

Dhima ya Matini Halisi Kufundishia Lg2 Kulingana na Utamaduni wa Lugha Husika

Uzingativu wa utamaduni unahusisha kuteua Matini Halisi zinazoonekana kuakisi utamaduni wa lugha anayojifunza mjifunzaji kwa wakati unaohusika. Mambo matatu muhimu ya kufikiriwa wakati wa kutumia Matini Halisi ambayo ni utamaduni, usasa na ukabilianaji na changamoto (Mshan, 2005). Miongoni mwa faida za kutumia Matini Halisi zilizongatia utamaduni wa lugha anayojifunzaji mjifunzaji zimeelezwa katika sehemu hii.

Kuhusianisha Moja kwa Moja Matini

Faida ya kwanza ya kutumia Matini Halisi ni kuwa mjifunzaji anahusianisha moja kwa moja matini anayoitumia na kile kitu anachojifunza. Kwa mfano, Matini Halisi ya *Gazeti la Mwanaspoti* iliyotumika kama kiolezo cha mada kuhusu mada ya mpira wa miguu nchini Tanzania. Anaposoma kipande cha habari katika gazeti hili kinachohusu mvutano wa mashabiki wa timu za Simba na Yanga kuhusu ubora wa usanifu wa jezi za timu hizi mbili, mjifunzaji anahusisha moja kwa moja timu na jezi na kile ambacho hukisikia au kukiona nje ya darasa. Hivyo, huwa rahisi kuhifadhi taarifa zake katika kumbukumbu za muda mrefu.

Uelewa wa Kujieleza kwa Urahisi

Faida ya pili ya kutumia Matini Halisi ni kwamba, mjifunzaji anapata uelewa wa kujieleza kwa urahisi. Matini Halisi zinazotumika zikiwa zimezingatia utamaduni wa lugha husika humpa fursa mjifunzaji kung'amua lugha na kuweza kujieleza kwa urahisi. Hali hii husababishwa na uhalisi unaoletwa na matini hiyo. Kwa mfano, *Gazeti la Mwanaspoti* linapotumika kama kiolezo cha kujifunzia habari za mchezo wa miguu nchini Tanzania yana uhalisi wa namna fulani. Ukiwa katika sehemu za starehe upo uwezekano mkubwa wa kusikia mvutano huo wa masuala ya usanifu wa jezi. Hivyo, mjifunzaji wa Lg2 anapofundishwa kwa kutumia Matini Halisi iliyozingatia utamaduni wa jamii, hupanua mweka wa uelewa na hivyo kuwa na fursa ya kuelezea jambo hilo kwa urahisi zaidi.

Kujifunza Lugha kwa Urahisi

Faida ya tatu ni kwamba mjifunzaji anajifunza kwa urahisi misamiati mipya kupitia maelezo au ufafanuzi uliomo katika Matini hizo. Kama ilivyofafanulia huko nyuma, Matini Halisi ni zile ambazo hazijarahisishwa. Zimetumia ufafanuzi wa undani kwa kuzingatia wazawa wanavyotumia lugha hiyo. Kwa mfano, katika mjadala wa usanifu wa jezi za timu za Simba na Yanga, maelezo ya mjazo yametolewa. Mathalani, kwa nini jezi ya timu X inasemekana ina misukule na ufafanuzi wa hiyo misukule. Ufafanuzi wa jezi ya timu Y kwamba ina makolokolo umetolewa kwa lugha ya mjazo. Hivyo, mjifunzaji wa Lg2 akijifunza kupitia Matini Halisi hiyo atapata maana za misamiati hiyo na mingine inayofungamanishwa na usanifu wa jezi za timu hizi.

Motisha ya Kujifunza Kupitia Matini

Jambo jingine ni kuwa mjifunzaji wa Lg2 anapata motisha ya kujifunza kupitia matini hizo. Tajiriba anayoipata kutoka katika hizo matini na mvuto wa vionjo vya

utamaduni vilivyoombatana na matini hayo humtia motisha ya kujifunza Lg2 anayojifunza. Kwa mfano, vipande vya habari kutoka katika *Gazeti la Mwanaspoti* kuhusu mvutano wa mashabiki wa timu za Simba na Yanga kuhusu usanifu wa jezi au hamasa ya Siku ya Wananchi au *Simba Day* vitamotisha mjifunzaji lugha kufuatilia matukio na shughuli ya timu hizi. Sababu ya kuibuka kwa motisha ni kutokana na usasa wa mambo yanayoelezwa katika habari hizi. Hoja ya usasa wa Matini Halisi ilipata kugusiwa na Mshan (2005) kama ilivyodokezwa hapo juu.

Kukuza Stadi za Lugha katika Hali ya Ung'amuzitambu

Mwisho, mjifunzaji wa Lg2 hukuza stadi za lugha katika hali ya ung'amuzitambu. Stadi kuu za lugha ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Utamaduni ni stadi mtambuka ambayo wajifunzaji wa Lg2 ni muhimu sana kujifunza. Hivyo, wajifunzaji wanapojifunza kwa kutumia Matini Halisi zilizotayarishwa kwa uzingatia utamaduni wa lugha husika, hung'amua stadi hizi kwa ufahamu. Utamaduni wa lugha huleta uhalisi wa lugha darasani. Kwa mfano, misamiati ya makorokoro, misukule, vibwengo, dera, birthday kutoka katika Matini za *Gazeti la Mwanaspoti* inaposomwa au kusikilizwa, mjifunzaji hupata ufahamu wa maana ya misamiati hiyo na muktadha ambamo hutumika tofauti na ingefundishwa kwa njia nyingine.

Uzingativu wa Utamaduni Wakati wa Utayarishaji Matini Halisi

Matini Halisi kama ilivyoielezwa hapo juu ni aina ya Matini zinazoweza kutumika kufundishia Lg2 ilhali hazikuandaliwa kwa lengo hilo. Hivyo, uteuzi wa aina za Matini Halisi zitakazochochea ujifunzaji wa Lg2 uweze kutokea ni uzingativu wa utamaduni wa lugha husika. Kama ilivyodokezwa, lugha na utamaduni vimefungamana pamoja na kwamba matini halisi ziwe ni zile zilizongatia lugha ya wakati huo. Lugha ya vijana ya wakati wa sasa, misemo na taswira mbalimbali ziwe ni zile zilizopo na kutumika mtaani kwa sasa. Matini Halisi ziwe ni zile zenye kuakisi utamaduni wa jamii ya makundi anuai kwa wakati wa sasa. Lengo ni kumsaidia mjifunzaji kuona kile kitu anachojifunza darasani, akitoka nje ya darasa apate kukisikia au kukihisi. Kwa mfano, tuseme mada inahusu *Mchezo wa mpira wa Miguu nchini Tanzania*. Katika mada hiyo, Matini Halisi inayoweza kufaa kufundishia mada hiyo ni *Gazeti la Mwanaspoti*. Vipande vya habari vya *Gazeti la Mwanaspoti* vinavyoonesha utani wa mashabiki wa timu za samba na Yanga kuhusu ubora na usanifu wa Jezi za timu hizo ni mwafaka kwa sababu ndiyo umebeba utamaduni halisi wa lugha ya michezo kwa mashabiki nchini Tanzania. Mjifunzaji wa Lg2 akijifunza kupitia matini hizo darasani, akitoka nje ya darasa anaweza kuhisi vionjo vya lugha hiyo kutoka kwa Watanzania na kumwezesha kuendelea kuibua ingizo zaidi la lugha anayojifunza.

Dumitrescu (2000) anasema kuwa Matini Halisi zinapochaguliwa na kutumika kwa umakini zinaweza kutayarisha shughuli ambazo zinaondoa mtazamo wa kuiangalia lugha kwa kuzingatia kanuni, badala yake kuwa ni daraja la kufikia malengo ya kiisimu na weledi. Mjadala utakaoibuka miongoni mwa wajifunzaji kuhusu muktadha uliokulia kuibuka kwa utani mashabiki wa timu za Simba na Yanga kuhusiana na usanifu wa jezi za timu zao kutampa uelewa mpana zaidi mjifunzaji lugha huyo

kuhusu lugha ya Kiswahili na utamaduni unaoambatana nayo. Matini hizo ni zile zilizingatia isimu, maana na utamaduni. Mshan (2005) akielekea kukubaliana na umuhimu wa uzingativu wa utamaduni katika kuteua na kutumia Matini Halisi katika madarasa ya Lg2 anasema mbinu za ufundishaji lugha kwa kutumia Matini Halisi zifungamanishe na utamaduni, usasa na ukabiliji wa changamoto.

Kwa upande wa usasa, Matini Halisi zidhihirishe hali ya lugha inayotumika na jamii kwa sasa. Tukirejelea mfano wa Matini Halisi za *Gazeti la Mwanaspoti* kuhusiana na mvutano wa mashabiki dhidi ya usanifu wa jezi za timu zao, hiyo ndiyo hali ya sasa na endelevu. Jezi hizi zinatengenezwa na kuzinduliwa kila mwaka. Matini hiyo itamwongezea motisha mjifunzaji wa kupenda kudadisi ziaid. Matini Halisi hiyo, haitaishia tu darasani; ataipata ndani na nje ya darasa. Kwa kufanya hivyo, atakuwa anapata ingizo thabiti la lugha anayojifunza. Mjifunzaji lugha atapata mwendelezo wa matukio haya ndani na nje ya darasa.

Kuhusu ukabilianaji na changamoto, huu ni ubashiri ambao unafanywa na mwalimu kuhusu aina ya changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa kutumia Matini Halisi kufundishia. Kufanya tafakari kuhusu uchangamani wa sarufi, misamiati na misimu anuai iliyotumika katika matini hiyo. Kwa mfano, katika utani wa mashabiki wa timu za Simba na Yanga kuhusu usanifu wa jezi za timu zao ipo misimu kadhaa mfano, *makorokoro, misukule, vibwengo, dera, birthday*. Mwalimu anaandaa mazingira ya ufafanuzi wa misimu hiyo. Kwa hiyo, kuhusu ukubilianaji wa changamoto za kutumia Matini Halisi kunahusu maandalizi ya kupitia Matini Halisi kabla ya kwenda kuitumia darasani na jinsi ya kuzikabili changamoto zinazoweza kuibuka.

Uhusiano na Uhalisi wa Matini za Kufundishia Lugha ya Pili

Dhana ya Matini Halisi katika taaluma ya ujifunzaji lugha ni pana na changamani. Kumeibuka mielekeo tofauti ya kinadharia kuhusu dhana ya uhalisi wa matini. Wataalamu wamekuja na violezo kuonesha Matini Halisi. Nunan (1997) anatazama dhana ya uhalisi wa matini kulingana na jinsi inavyotumika katika zoezi la ufundishaji wa lugha. Anapendekeza uhalisi utafsiri kulingana na jinsi matini husika inavyotumika katika zoezi la kufundisha lugha darasani. Hivyo, anapendekeza aina tano za uhalisi wa matini. Aina hizo ni uhalisi wa malengo, mazingira, matini, matendo na uhalisi wa mjifunzaji wa uhalisi fuluni. Matini ni halisi kwa mjifunzaji ikiwa zinakubalika darasani, zinagusia hisia za mjifunzaji lugha, historia ya mjifunzaji, matarajio na matamano ya mjifunzaji. Uhalisi wa matini unategemea zaidi mwitikio wa mjifunzaji kuhusu matini hiyo, ikiwa anaiona inamsaidia kupata kitu kipya kuhusiana na lugha.

Richards (2001) alipendekeza aina mbili za uhalisi wa matini. Matini Halisi hazijaandaliwa kwa ajili ya kufundishia Lg2. Matini zisizohalisi, hivi ni vitabu vya kiada na vifaa vingine vilivyotayarishwa maalumu kwa ajili ya kutumika kufundishia Lg2. Richard anasema Matini Halisi ndizo zitumike darasani kwa sababu huleta ulimwengu halisi darasani. Jordan (2012) anatazama uhalisi wa matini za kujifunzia na kufundishia lugha katika mielekeo minne ambayo ni ingizo la lugha, shughuli,

tukio na tajiriba ya mjifunzaji lugha. Kisha, anaangalia masuala ya ukweli wa matini hizo na kama zililenga kutumika kufundishia lugha katika muktadha wa darasani. McKay (2013) anafafanua uhalisi wa Matini kwa kurejelea maudhui yaliyomo katika matini kwa ajili ya mawasiliano kwa ujumla na siyo tu wanalugha wa lugha anayojifunzaji mjifunzaji. Pili, maingiliano yaliyolenga kumwandaa mjifunzaji kukabiliana na ulimwengu halisi wa lugha nje ya muktadha wa darasa. Uhalisi wa lugha maana yake siyo kuhusianisha mambo ya darasani na yale ya nje ya darasa tu, kwa kuwa darasa ni jumuiya ambapo wajifunzaji lugha hupewa fursa za kuchangamana na matini kuhusu mambo muhimu ya kwao.

Jiuhan na wenzake (2011) wanasema Matini Halisi zinaweza kugawanywa katika mielekeo mikuu mitano. Mosi, Matini za ajira zenye mielekeo ya ajira, kutafuta kazi, kufungua kampuni, kuomba ajira na zinazohusu mahojiano/usaili. Pili, Matini za teknolojia na anuanipepe, mtandao, matini za kusikiliza, luninga au simu. Tatu, Matini za bidhaa, zinazohusu orodha ya bidhaa, matangazo, nembo, maombi na brosha za taasisi. Nne, Matini za huduma kwa wateja zinazohusu maelekezo ya vifungashio vya dawa, taarifa kuhusu huduma za dharura, huduma za usafiri na usafirishaji kama vile ramani na ratiba, machapisho kuhusu uendeshaji magari, matini zenye kuhusiana na habari, kwa maana ya: makala, vikatuni na ripoti maalumu, matangazo na taarifa za benki na atini zinazohusu uraia na ushiriki wa raia katika shughuli mbalimbali zinazohusu vifaa na taarifa kuhusu uraia, vifaa na taarifa kuhusu ushiriki wa raia.

Goode, Sockalingam, Brown na Jones (2000) wanafasili dhana ya utamaduni kuwa ni mwingiliano wa ruwaza anuai za tabia ya binadamu zikijumuisha fikra, mawasiliano, lugha, mazoezi, thamani, mila na desturi, mwenendo wa maisha. Utamaduni ndiyo hudhibiti namna ya kuchangamana kijamii na jinsi ya kuukabili ulimwengu unaotuzunguka. Wajifunzaji wa Lg2 ni vigumu kujifunza vipengele vyote hivyo katika kipindi kimoja, bali huendelea kujifunza katika muda wao wote wa masomo. Utamaduni huendelea kuathiri zoezi la kujifunza Lg2. Lugha huwezesha kuhamisha habari, mawazo na namna ya kuwasilisha fikra au mawazo tunayofikiria. Utamaduni ndiyo huukilia lugha inayozungumzwa au kuandikwa katika jamii. Kama wajifunzaji wa Lg2 watafundishwa maarifa ya utamaduni wa lugha wanayojifunza kwa njia ya uzamajikindakindaki katika mazingira ya kijamii yenye utamaduni toshelevu wa lugha wajifunzayo na kuchangamanishwa na vifaa zilizosheheni utamaduni Lg2, kuna uwezekano mkubwa wa kujifunza lugha hiyo kwa haraka, rahisi na ufanisi mkubwa. Maandalizi ya Matini Halisi yanayozingatia na kufumbata utamaduni wa lugha husika yatakuwa yanawakilisha lugha halisi inayotumika kwa wakati huo.

Hitimisho

Makala haya yanahitimishwa kuwa uhalisi wa matini za kujifunzia na kufundishia Lg2 udhihirike katika matini husika. Lugha iliyotumika kuzitayarisha matini hizo iwe ni ile inayotumiwa na jamii wakati husika yenye kuakisi makundi mbalimbali ya kijamii yaliyomo ndani ya jamii lugha hiyo. Kwa kuwa wajifunzaji wa Lg2 hujifunza lugha kwa lengo mawasiliano, matini za kujifunzia Lg2 zifumbate stadi kuu za lugha,

kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Hizi matini ziwe halisi kwa kuzingatia stadi muhimu za lugha za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Kuna vipengele vingine vya kuzingatiwa wakati wa uteuzi wa Matini Halisi za kufundishia kama vile msamiati, sarufi na utamaduni wa lugha. Matini hizi zibebe maudhui ambayo yanaendana na wanafunzi. Matini Halisi zizingatie usuli wa kihistoria wa wajifunzaji. Matini Halisi, humwezesha mjifunzaji lugha kuchangamana na lugha halisi na si tu miundo na sarufi ya lugha. Matini Halisi huwezesha kuimarika kwa umilisi wa kimawasiliano wa mjifunzaji, hasa umilisi wa kiisimu, umilisi wa kiisimujamii, umilisi wa kipragamatiki, umilisi wa kimkakati na umilisi wa kilongo.

Marejeleo

- Brown, H. D. (2014). *Principles of Language Learning and Teaching: A Course in Second Language Acquisition*. New York: Pearson Education, Inc.
- Dumitrescu, V. (2000). Authentic Materials: Selection and Implementation in Exercise Language Training, *English Teaching Forum*, 38(2), 20-25.
- Ellis, R. (1999). Item versus system learning: explaining free variation, *Applied Linguistics*, 20: 460-80.
- Garton, S., na Graves, K. (2014). Materials in ELT: Current Issues, Katika S. Garton na K. Graves (Wah.), *International Perspectives on English Language Teaching*. London: Palgrave Macmillan.
- Gass, M. S., na Mackey, A. (2015). Input, Interaction, and Output in Second Language Acquisition. Katika Van Patten na Williams (Wah.). *Theories in Second Language Acquisition: An Introduction* (2nd Edition). Routledge: New York. Kur 180-206.
- Gilmore, A. (2007). Authentic Materials and Authenticity in Foreign Language Learning, *Language Teaching*, 40 (02), 97-118.
- Gilmore, A. (2008). Getting Real in the Language Classroom: Developing Japanese Students' Communicative Competence with Authentic Materials. Tasnifu ya Uzamivu. Imepakuliwa kutoka <http://eprints.nottingham.ac.uk/11928/1/478936.pdf>.
- Goode, T., Sockalingam, S., Brown, M., & Jones, W. (2012). *A Planner's Guide. Infusing Principles, Content and Themes Related to Cultural and Linguistic Competence into Meetings and Conferences*. Washington, DC: Georgetown University Center for Child and Human Development, National Center for CulturalCompetence.
- Grellet, J. (1981). *Developing Reading Skills*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Hall, G. (2011). *Explaining English Language Teaching: Learning in Action*. London: Routledge.
- Howard, J., na J. Major. (2004). *Guidelines for Designing Effective English Language Teaching Materials*. Imepakuliwa kutoka <http://www.paaljapan.org/resources/proceedings/PAAL9/pdf/Howard.pdf>. Kur. 101-109.

- Hutchinson, T., na Waters, A. (1987). *English for Specific Purposes: A Learning-Centred Approach*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Jiuhan, H., Tindall, E., na Nisbet, D. (2011). Authentic Activities and Materials for Adult ESL Learners, *Journal of Adult Education*, 40(1), 1-10.
- Jordan, R. R. (2012). *English for Academic Purposes: A guide and Resource Book for Teachers*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Krashen, S. D. (1985). *The Input Hypothesis: Issues and Implication*. New York: Longman.
- McGrath, I. (2013). *Teaching Materials and the Roles of EFL/ESL Teachers: Practice and Theory*. London: Bloomsbury.
- McKay, S. (2013). Authenticity in the Language Teaching Curriculum, C.A. Chapelle (Mh.), *The Encyclopedia of Applied Linguistic*, 1-6. New York: Blackwell Publishing Ltd.
- Mishan, F. (2005). *Designing Authenticity into Language Learning Materials*. Bristol: Intellect Books.
- Nunan, D. (1997). Designing and Adapting Materials to Encourage Learner Autonomy, katika P. Benson na P. Voller (Wah.), *Autonomy and Independence in Language Learning*, 192-203). London: Longman.
- Pinner, R. (2015). What We Talk About When We Talk About Authenticity: *UniLiterate*. Imepakuliwa kutoka <http://uniliterate.com/2015/05/talk-talk-authenticity>.
- Pinner, R. S. (2014). The Authenticity Continuum: Towards a Definition Incorporating International Voices. Katika *English Today*, 30(4): 22-27.
- Richards, I., na Rodgers, T. (1986). *Approaches and Methods in Language Teaching*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Richards, J. C. (2001). *Curriculum Development in Language Teaching*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Rilling, S., na Dantas-Whitney, M. (2009). *Authenticity in the Language Classroom and beyond: Adult learners. Classroom Practice*. Virginia, USA: TESOL Inc.
- Rubin, J. (1979). What the good Language Learner can Teach Us, J.B. Pride (Mh.), *Sociolinguistic Aspects of Language Learning and Teaching*, Oxford: Oxford University Press.
- Scrivener, J. (2011). *Learning Teaching: The Essential Guide to English Language Teaching. Toleo la 3*. UK: Macmillan Education.
- Tomlinson, B. (1998). *Materials Development in Language Teaching*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Widdoson, H. G. (1978). *Teaching Language as Communication*. Oxford: Oxford University Press.

Widdoson, H. G. (1979). *Explorations in Applied Linguistics*. Oxford: Oxford University Press.

Wright, T. (1987). *Role of Teachers and Learners*. Oxford: Oxford University Press.